# LATRA yaanza kung'ata, daladala 45 zakamatwa kwa kupandisha nauli Arusha

**NA JOSEPH NGILISHO, ARUSHA**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Kanda ya Arusha, imeanza operesheni ya kukabiliana na wamiliki na madereva wa daladala wanaokiuka viwango vya nauli vilivyowekwa na serikali, ambapo zaidi ya gari 45 zimekamatwa na kutozwa faini kali.

Hatua hiyo imekuja sambamba na onyo kali la kufungiwa leseni kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri watakaoendelea kukaidi maelekezo ya serikali.

Utekelezaji wa nauli mpya za daladala jijini Arusha ulianza Mei Mosi mwaka huu, ukiwa na lengo la kudhibiti ongezeko holela la nauli na kulinda maslahi ya abiria.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Usafirishaji, Omari Ayubu, alisema viwango hivyo vipya vimepangwa kwa kuzingatia umbali wa safari ili kuhakikisha haki na usawa kwa watumiaji wa usafiri wa umma.

Alieleza safari zisizozidi kilomita 10 zitatozwa shilingi 700, huku safari za hadi kilomita 15 zikitozwa shilingi 800.

"Katika jiji la Arusha, safari nyingi zinaangukia katika viwango hivi, hivyo wananchi wengi watanufaika na mfumo huu mpya wa nauli," alisema.

Alitoa mfano kuwa abiria wanaosafiri kutoka Chekereni au Moshi hadi stendi ndogo umbali wa takribani kilomita saba wanapaswa kulipa shilingi 700, huku wanaovuka maeneo kama Relini kuelekea katikati ya jiji wakitakiwa kulipa shilingi 800.

Kwa mujibu wa Ayubu, serikali pia imeelekeza daladala zote kubandika jedwali la nauli, ndani ya gari ili kuongeza uwazi na kupunguza migogoro kati ya abiria na wahudumu.

"Hatua hii itasaidia kila abiria kufahamu kiwango halisi cha nauli na hivyo kupunguza ubishani usio wa lazima," alisisitiza.

Hata hivyo, licha ya kuanza kwa utekelezaji huo, baadhi ya madereva na makondakta wameendelea kupuuza viwango hivyo, hali iliyosababisha kuanzishwa kwa ukaguzi mkali barabarani.

Alisema ndani ya wiki moja, zaidi ya gari 45 zimekamatwa kwa kosa la kutoza nauli zaidi ya kiwango kilichowekwa.

"Kutoza nauli zaidi ya iliyoelekezwa ni kosa la kisheria. Hatutasita kuchukua hatua kali, ikiwemo kusimamisha huduma kwa wahusika," alionya.

Aidha, aliwataka abiria kudai haki zao wanapolipa nauli, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapewa chenji sahihi.

"Ni dhuluma kumnyima abiria chenji yake. Wananchi wasisite kudai haki zao," alisisitiza.

Katika kuimarisha usimamizi, serikali imewahimiza wananchi kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu madereva na makondakta wanaokiuka taratibu, kupitia namba maalum zilizotolewa.

Wakati huo huo, baadhi ya viongozi wa serikali wakiwemo wakuu wa wilaya wameanza kushuka barabarani kusimamia utekelezaji wa viwango hivyo, hatua inayolenga kuhakikisha sheria zinafuatwa kikamilifu.

Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya serikali na wananchi ili kufanikisha mfumo huo mpya wa nauli.

Akizungumzia malalamiko kuhusu nauri usafiri wa bajaji alifafanua kuwa vyombo vya usafiri wa kukodisha kama bajaji, bodaboda na teksi, hutumia mfumo wa makubaliano kati ya dereva na abiria katika kupanga nauli.

Hali hiyo inamaanisha kuwa nauli za bajaji zinaweza kutofautiana kulingana na maelewano ya pande mbili.

"Mfano, leo dereva anaweza kutoza shilingi 500 na kesho shilingi 2,000, kulingana na makubaliano. Hii ni kwa sababu bajaji ni usafiri wa kukodisha," alisema

Kutokana na changamoto ya usafiri, mamlaka imeanza kupanua huduma za daladala katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakitegemea zaidi bajaji, ili kuwapa wananchi chaguo la usafiri kwenye nauli elekezi na nafuu.

Wananchi wametakiwa kuelewa kuwa wanapochagua kutumia bajaji, wanakuwa wamekubaliana na masharti ya nauli kwa hiari yao, tofauti na daladala ambazo zinafuata viwango rasmi vilivyowekwa na serikali.

Mamlaka imewataka wananchi katika maeneo ambayo bado hayana huduma ya daladala kutoa taarifa ili hatua zichukuliwe haraka kuimarisha upatikanaji wa usafiri wa uhakika na wa gharama nafuu.

CamScanner

Mwananchi Jumatano Mei 6, 2026 Pg 3

# Nauli za bajaji zapaa Moshi, wananchi waiangukia serikali

Janeth Joseph, Mwananchi
jjoseph@mwananchi.co.tz

**Moshi.** Wakati bajaji zikiendelea kufanya biashara kama daladala katikati ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, baadhi ya wananchi wamelalamikia kupandishiwa nauli kiholela, hali inayowafanya baadhi ya wananchi wenye kipato cha chini kushindwa kumudu gharama.

Bajaji hizo, ambazo zimesajiliwa kama chombo cha usafiri wa kukodi, zimegeukia biashara hiyo baada ya kuondolewa kwa daladala katika njia zote za manispaa hiyo, na hivyo wananchi kukosa usafiri mbadala.

Kutokana na kukosekana kwa usafiri wa umma (daladala), wananchi hao wamejikuta wakilazimika kulipa nauli kati ya Sh1,500 badala ya Sh700, na Sh5,000 badala ya Sh3,000 kwa mtu mmoja.

Hayo yanatokea licha ya Serikali kutangaza bei elekezi ya nauli kuanzia Mei mosi mwaka huu, ambapo kwa usafiri wa daladala imeongezeka Sh100, na hivyo kufanya nauli kupanda kutoka Sh600 hadi Sh700 kwa umbali usiozidi kilomita 10.

Awali, wananchi hao walikuwa wakitumia daladala kabla bajaji hazijaingia mjini, na baadaye daladala hizo zilishindwa kufanya usafirishaji kutokana na ushindani uliokuwapo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wananchi hao wameiomba Serikali kuingilia kati hali hiyo, ili kudhibiti bei hizo na kuwatafutia usafiri wa umma (daladala), wakieleza kuwa wanashindwa kumudu gharama za bajaji kutokana na baadhi ya madereva kupandisha nauli.

> **"Kama bajaji zimeamua kufanya usafiri wa umma, kwanini hazizingatii bei elekezi ambayo Serikali imetoa, ambapo imeongezeka Sh100 tu? Tunaomba Serikali itusaidie."**
>
> Mkazi wa Moshi, Germana Joseph

Germana Joseph, mkazi wa Manispaa ya Moshi, alisema gharama za usafiri wa bajaji zimekuwa kubwa kutokana na kukosekana kwa daladala, hali inayowapa mzigo mkubwa wananchi wenye kipato cha chini.

"Nauli ilikuwa ni Sh700 kutoka mjini hadi Msaranga, baada ya mafuta kupanda, bajaji wametupandishia nauli hadi Sh1,500. Huu ni mzigo kwetu.

"Kama bajaji zimeamua kufanya usafiri wa umma, kwanini hazizingatii bei elekezi ambayo Serikali imetoa, ambapo imeongezeka Sh100 tu? Tunaomba Serikali itusaidie, wananchi tunateseka," alisema mwananchi huyo.

Mwananchi mwingine, Jasmin Ally, mkazi wa Kahe, alisema awali nauli ilikuwa Sh3,000, lakini sasa imepandishwa hadi Sh5,000.

"Bajaji za huku Kahe tunapanda hadi watu sita badala ya watatu, na nauli unalipa hiyo hiyo. Yaani tumepandishiwa nauli kutoka Sh3,000 hadi Sh5,000 kwa mtu mmoja, kwenda na kurudi mjini ni Sh10,000. Huyu mwananchi wa kawaida anapata wapi hii nauli kila siku?" alihoji Ally.

Yustela Moshi ameiomba Serikali kuingilia kati na kuangalia namna ya kudhibiti upandishwaji wa nauli hizo kiholela, akisema baadhi yao wanalazimika kutembea kwa miguu kutokana na gharama kuwa kubwa.

Akizungumzia hilo, Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bodaboda na Bajaji Manispaa ya Moshi, Hamadi Bendera, alisema wamepokea malalamiko kutoka kwa wananchi, na kwamba watakaa na kuona namna ya kuweka nauli rafiki.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliwataka madereva wa bajaji kuzingatia bei elekezi iliyotolewa na Serikali, na kumwagiza Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Usafiri Ardhini (Latra) mkoani humo kufuatilia suala la upandaji wa nauli kiholela.

CamScanner

Mhariri,


Kondakta wa daladala akizozana na abiria.

# Ni wajibu wa kondakta kutafuta chenchi

NINAANDIKA barua hii kuwasilisha kero inayowakumba abiria wengi wa daladala katika Jiji la Dar es Salaam, hususan baada ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kupandisha nauli.

Kumekuwepo tabia iliyozoeleka kwa baadhi ya makondakta kutorudisha chenchi ya shilingi 100 kwa abiria, jambo ambalo linaonekana dogo kwa macho ya haraka, lakini kwa uhalisia wake lina athari kubwa kwa wananchi wa kipato cha chini.

Ni jambo la kushangaza kuona kuwa abiria analipa nauli kamili kwa kutumia noti kubwa au sarafu aliyonayo, lakini anapodai chenchi yake, anaahidiwa kupewa baadaye bila kutekelezwa.

Ni kawaida kumsikia kondakta anapodaiwa chenchi kusema; "subiri chenchi yako nitakupa". Wakati mwingine makondakta hujifanya kusahau au kupuuza kabisa madai ya abiria. Hali hii imekuwa kama utaratibu usio rasmi unaoendelea kila siku bila kudhibitiwa.

Hali hii imeishuhudia wakati natokea Kinyerezi kwenda Mnazi Mmoja ambapo nauli ni shilingi 900, abiria alitoa Sh. 1,000 ya noti hivyo alitakiwa kurejeshewa chenchi ya Sh. 100 lakini kondakta akamzungusha abiria hadi aliposhuka bila kupewa kwa kigezo kuwa hana chenchi.

Kwa mtazamo wa haraka, shilingi 100 inaweza kuonekana siyo kiasi kikubwa.

Hata hivyo, tukizingatia idadi ya abiria wanaosafiri kila siku na kukosa haki yao ya chenchi, fedha hiyo hukusanyika na kuwa kiasi kikubwa kinachowanufaisha watu wachache kwa njia isiyo halali.

Zaidi ya hapo, kwa wananchi wanaopambana na hali ngumu ya maisha, kila shilingi ina thamani na umuhimu wake.

Tatizo hili pia linaashiria kukosekana kwa uwajibikaji na nidhamu katika sekta ya usafiri wa umma.

Abiria wanaponyimwa haki yao ya msingi, hujenga hisia za kukosa haki na kudharauliwa.

Aidha, hali hii inaweza kusababisha migogoro isiyo ya lazima kati ya abiria na wahudumu wa daladala, jambo ambalo linaweza kuepukika kabisa kama kila upande utazingatia wajibu wake.

Ni rai yangu kwa mamlaka husika, hususan LATRA na vyombo vya usimamizi wa usafiri, kuchukua hatua madhubuti kudhibiti tabia hii.

Ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike, na hatua zichukuliwe dhidi ya makondakta na madereva wanaokiuka taratibu. Aidha, elimu itolewe kwa wahudumu wa daladala kuhusu umuhimu wa kuwaheshimu abiria na kutoa huduma kwa uadilifu.

Vilevile, abiria nao wanapaswa kuwa na ujasiri wa kudai haki yao kwa njia ya staha na kufuata taratibu. Pale ambapo haki haitolewi, ni vyema kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili hatua zichukuliwe.

Ushirikiano kati ya abiria na mamlaka unaweza kusaidia kukomesha tabia hii isiyofaa.

Kwa ujumla, kurejesha chenchi si hisani bali ni haki ya abiria.

Ni wakati sasa wa kuhakikisha kuwa haki hii inaheshimiwa ili kuboresha huduma ya usafiri wa umma na kujenga mazingira ya kuaminiana kati ya wahudumu na watumiaji wa huduma hizo.

**Salma Omary,**
**Kinyerezi, Dar es Salaam.**